**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KAGERA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI YA SERIKALI NKWENDA

**Juni, 2024**

**NKWENDA -KYERWA DC**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**


**Namba za Sim 0783302024**

**Mkuu wa Shule 0783302024**

**Makamu Mkuu wa Shule**. **0752828879**

**Mwalimu malezi ; 0768261128**

**Shule ya Sekondari** Nkwenda,

**S.L.P. 417**

Kyerwa.


**31/05/2024.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi .............................................**
**..................................................................**
**S.L.P ........................................................**
**....................................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NKWENDA HALMASHAURI (W) KYERWA MKOA KAGERA MWAKA 2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya CBG

Shule ya Sekondari Nkwenda sekondari ipo umbali wa Kilometa 2 Kusini mwa Mji wa Nkwenda Usafiri wa pikipiki kutoka mjini nkwenda unapatikana katika kituo cha mabasi nkwenda Nauli ni Shilingi 1500.00

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 28/06/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 10/07/2024.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni kwa Wasichana sketi mbili (2) za rangi nyeusi za lindabox (linda moja kubwa yaani katikati,mbele na nyuma)marinda mawili madogo mkono wa kulia na wa kushoto baada ya lindabox. upana wa marinda ni inchi mbili ( knife edge pleats ) upana wa mkanda usiozidi inchi mbili .sketi iwe na urefu wa kutosha inchi kumi chini ya magoti , kiwe kitambaa kizito.

ii. Mashati 02 meupe ya mikono mirefu.

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe kwa waislamu na kitambaa ndani ya kijuba kiwe cheupe na awe na zaidi ya kimoja.

iv. Sare ya Michezo aje na truck suit rangi ya dark blue na viatu vya raba.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na viwe vya ngozi.

vi. Stocking jozi mbili nyeupe

vii. Sweta maalumu za rangi ya dark blue

ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) Gauni 02 za blue na ndefu inchi kumi chini ya magoti.

ix. Tai 02 za rangi damu ya mzee yenye michirizi mieupe

x. Tisheti 01 (T-shirt) rangi ya blue yenye kola isiyochangamana na rangi nyingine na isiwe na maandishi.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari ya kutosha Masomo

ii. Ream (A4) ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka kila Muhula ni rimu 1

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Scientific Calculator; (zinapatikana kwenye mazingira ya shule kwa bei ya Tsh 35000/=)

vi. Godoro 1 la nchi 2 na nusu kwa 6
vii. Mashuka Jozi 2 ya pink , blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
viii. Nguo za ndani za kutosha na night dress
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 (moja kubwa(lita ishirini) na ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mfagio 1 wa nje na brush 1.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ................**
**Jina la Mkuu wa Shule:CYLIVANUS K. BALYAMWAGIRA.**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule ................**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0783302024**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0752828879**
- **Mwandamizi Taaluma 0788422227**
- **Mwandamizi Malezi 0787577368**

## SHULE YA SEKONDARI NKWENDA
## FOMU YA KUKUBALI NA KUTII SHERIA ZA SHULE

ANWANI...........................................................................................

Mimi................................................................ (Jina la mwanafunzi) nimepokea barua ya kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari Nkwenda kuanzia tarehe 13/08/2024 hadi 31/08/2024. Nakubali nafasi hiyo kwa moyo mkunjufu. Baada ya kusoma na kuelewa sheria za shule, naahidi kuwa nitatii sheria hizo kama zilivyoainishwa katika fomu ya maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Nkwenda. Endapo nitashindwa kutii sheria hizo hatua inayostahili ichukuliwe dhidi yangu .Natoa ahadi hii mbele ya Mzazi /mlezi wangu ambaye ametia sahihi yake hapa chini.

Jina la mwanafunzi .......................................... sahihi...........................................

Mimi................................................................ (Jina la mzazi /mlezi) ambaye ni mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu, nakubali mwanangu ajiunge kidato cha tano katika shule ya sekondari Nkwenda na kutii sheria za shule na naahidi kushirikiana na shule ili kuhakikisha tunatoa malezi bora kulingana na sheria hizo na nyingine ambazo hazikutajwa pia.

Iwapo sitakuwepo mimi likitokea tatizo ninaweza kuwakilishwa na

1. .................................................... ambaye ni ............................................

2. ...................................................... ambaye ni ..................................................

(Eleza uhusiano wako na wawakilishi hao)..........................................................

Sahihi ......................................................

Tarehe............................................................

**SHULE YA SEKONDARI NKWENDA**

**KIAMBATANISHO B**

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI..................................................... (Kama ilivyo kwenye Selform)
2. Tarehe ya kuzaliwa...................................................
3. Mahali alipozaliwa: Wilaya...................Kijiji ................. kata ..........................
4. Anwani ya nyumbani ni ...................................................
5. Dini yake ..................................................................

**WAZAZI**/MLEZI

Jina …..................................... Anwani ................................................ Anaishi /Amefariki (kata isiyohusika)..................................................

Ni raia wa nchi ipi? Itaje ................................................ (Tanzania/nchi nyingine)

**MAELEZO YA AFYA**

Eleza kama una tatizo lolote linalohitaji msaada au linaloweza kuathiri utendaji wako wa kazi za kila siku pamoja na maendeleo yako ya masomo. Maombi maalumu yadhibitishwe na daktari.

.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.

**SHULE YA SEKONDARI NKWENDA**

**KIAMBATANISHO C**

**HATI YA UTHIBITISHO WA TABIBU (anayetambuliwa na serikali)**

Nathibitisha kwamba nimemchunguza mwanafunzi

Jina: .......................................................

Kinyesi...................... Matokeo........................................................

Mkojo.................... Matokeo........................................................
Macho.................... Matokeo.............................................

Damu.................... Matokeo............................................
Mapigo ya moyo.................... Matokeo............................................
Urine Pregnancy Test (UPT).................... Matokeo.............................................
Matatizo mengine kama yapo....................

**MATIBABU** Yafuatayo yametolewa (kama ni ugonjwa wa kudumu eleza)
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.......................................................................................................................................
.........................................................................
Jina la tabibu: ........................................................Sahihi: ....................................

Tarehe.............................................................

Muhuri............................................................

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**

**SHULE YA SEKONDARI NKWENDA**

**S.L.P 417 KYERWA.**

**FOMU YA TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

**1.TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI.**

Jina la mwanafunzi ......................................................jinsi..................Tarehe ya kuzaliwa…........................

Shule ya Sekondari aliyotoka ......................................................................

Jina la baba.............................kazi yake.........................Simu............................

Jina la mama ......................................kazi yake...................................Simu...............................

Kijiji/mtaa wanapoishi.....................................Wilaya ...........................Mkoa.....................................

Dini…........................................................................................

Majina ya ndugu wa karibu wa mawanafunzi .;

....................................................................anakoishi...................................simu..............................

..............................................................anakoishi..............................................simu................................

.anakoishi.............................................simu....................................................

**2.KUKUBALI NA KUTII SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE.**

Mimi (Jina la mwanafunzi)................................................naahidi sitashiriki kabisa katika fujo /migomo na kutenda makosa ya jinai shuleni na maeneo mengine .Pia naahidi kuzifuata sheria na taratibu zote za shule kwa faida yangu binafsi ,kwa shule na kwa Taifa kwa ujumla .Endapo nitakwenda kinyume na taratibu,kanuni na sheria za shule nakubali kufukuzwa shule au ksimamishwa masomo na kupewa adhabu nyingine kulingana na sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na sheria ya makosa ya jinai ya mwaka 2002.

**JINA LA MWANAFUNZI........................................... SAINI...................................TAREH......................**

**JINA LA MZAZI............................................SAINI.......................................TAREH.......................**

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**

**SHULE YA SEKONDARI NKWENDA**

**S.L.P 417-KYERWA**

**..............................................................................................................**

**FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI**

MGANGA MKUU/MGANGA MFAWIDHI

KITUO CHA AFYA/ HOSPITALI

.....................................................

......................................................

............................................................

**YAH: KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI ....................................................................KWA AJILI YA KUJIUNGA NA SHULE.**

Kijana huyu amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii Kamuli Sekondari ,hivyo naomba uthibitishe hali ya afya yake kabla ya kuanza masomo yake hapa shuleni kwa haya yafuatayo;

**1. TB.........................................................................................................................**

**2. HB.........................................................................................................................**

**3. STOOL.....................................................................................................................**

**4. URINE.....................................................................................................................**

**5. EYE/EARS.................................................................................................................**

**6. ATHMA.....................................................................................................................**

**7. TYPHOID..................................................................................................................**

**8. OTHERS...................................................................................................................**

**OREDHA YA VITABU AMBAVYO MZAZI ANAWEZA KUVINUNUA KWA AJILI YA MWANAE KUJISOMEA YEYE BINAFSI.**

## ADVANCED LEARNERS DICTIONARY (OXFORD)

**a. Chemistry**

i). Advanced level organic chemistry by APE network 2012 ii). A' level secondary Education chemistry practical iii). Advanced inorganic chemistry volume I and II by S. CHAND iv). Environmental chemistry and pollution control by S. CHAND v). Essential physical chemistry by S. CHAND vi). Selected topics in inorganic chemistry by Wahid U. Malik et al vii). Organic chemistry by S. CHAND

**Biology**

i). CJ CLEGG with DG MACKEAN (2000) Advanced Biology principles and Application 2nd Ed,

Hodder Murray London ii). Sylvia S Mader (1996), Biology ( 5th Ed ) Wm C. Brown publisher London iii). DJ Taylor et al (1997), BIOLOGICAL SCIENCE, Cambridge university press – New York.

iv). MBV Roberts (1986), Biology A functional Approach ( 4th Ed )

v). Ann Fullick et al (2011), A level Biology, students Book, Longman. **d.**

**General studies**

i). General studies for A' level certificate form v by. RICHARD R MBALASE ii). General studies for A' level certificate form vi. By RICHARD R. MBALASE e.

**Geography**

i). Practical geography Alive by Zisti

- Map Reading, photography Interpretation, Field Research, Statistics, and Survey Illustrated by Ellias Anthony Mkoko
- Affordable Edition for secondary and High school learners kot publishers ii). A comprehensive approach to physical geography by D.T. Msabila iii). Human and Economical Geography by Gillan C. Morgan iv). Soil and Climatology by Zisti **f.**

## GENERAL STUDIES

1. Richard, R.F. Mbalase. General Studies For Advanced Level Certificate;
2. Mgaywa, B.M. General Studies for Advanced level 3rd Ed.
3. Joannes BigirwaMungu & Sospeter.M. Deogratias. Understanding Advanced Level general Studies;

## GEOGRAPHY DEPARTMENT

1. (colin Buckle), LANDFORMS IN AFRICA

2. C.R. KOTHARI), RESEARCH METHODOLOGY

3. (H.c. TRURAN), A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAPS AND DIAGRAMS

4. (Goh Cheng Leong.Gillian.C. Morgan), HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY

5. (DAVID WAUGH), GEOGRAPHY-AN INTIGRATED APPROACH.